**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

**MTIHANI WA KUFUNGA NUSU MUHULA WA 1 MACHI, 2024**
**KIDATO CHA NNE – KISWAHILI**

**MUDA: SAA 3** **MARCHI 2024**

**Maelekezo:**

1. Mtihani huu una sehemu tatu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi (10).
2. Epuka kuleta vitu visivyoruhusiwa katika chumba cha mtihani kama vile simu, karatasi,vitabu, madaftari, vikokotozi, n.k
3. Zingatia maelekezo uliyopewa kwa kila sehemu na kila swali.
4. Kumbuka kuandika majina yako kwa usahihi katika kila karatasi uliyojibia.
5. Udanganyifu wa aina yoyote ile utakupelekea ufutiwe mtihani au kupunguziwa alama.
6. Sehemu 'A' in ajumla ya alama 16 yenye maswali mawili (2), sehemu 'B' in alama 54 yenye maswali sita (6) wakati sehemu 'C' yenye maswali mawili (2) in alama 30.
7. Jibu maswali yote katika sehemu zote A, B na maswali mawili tu (2) katika sehemu C. swali la 10 ni LAZIMA.

**SEHEMU A: (ALAMA 16)**

1. Chagua jibu lililo sahihi kati ya majibu matano uliyopewa kisha andika HERUFI ya jibu ulilochagua,kuanzia swali (i) hadi (x).

i) Katika upatanisho wa kisarufi, neno "bati" linaingia katika ngeli ipi?
A. I – ZI
B. U – ZI
C. U – YA
D. KI – VI
E. LI – YA

ii) Kipashio kinachokamilisha taarifa ya kitenzi kisichokuwa na uarifishaji kamili katika sentensi hujulikana kama;
A. Kijalizo
B. Shamirisho
C. Kiarifu
D. Changizo
E. Prediketa

iii) Utofauti wa kiamtamshi, kimaumbo na matumizi ya maneno katika lugha kuu moja katika maeneo mbalimbali huitwa;
   A. Misimu
   B. Lahaja
   C. Rejesta
   D. Lafudhi
   E. Kiimbo

iv) Neno LUKU hutumiwa na TANESCO pamoja na wateja wa umeme. Je, neno hilo limeundwa kwa njia gnai?
   A. Akronimu
   B. Uambishaji
   C. Ukopaji
   D. Uhulutishaji
   E. Utohoaji

v) Ni aina ipi ya usomaji huweza kupima umahiri wa kutamka maneno kwa ufasaha na kutumia lafudhi sahihi ya lugha ya mhusika?
   A. Kusoma kwa burudani
   B. Kusoma kimya
   C. Kusoma kwa sauti
   D. Kusoma kwa makini
   E. Kusoma kwa mkazo zaidi

vi) Mbinu ya pekee inayomwezesha msanii wa kazi ya fasihi kuwa tofauti kabisa na mwingine ni ipi?
   A. Utumizi wa lugha
   B. Muundo
   C. Mandhari
   D. Husuka wahusika
   E. Mtindo

vii) Sababu ipi kati ya hizi haihusiki na uundaji wa maneno katika lugha?
   A. Kukuza lugha husika
   B. Kuibuka kwa mambo mapya katika jamii
   C. Kukidhi mahitaji ya mawasiliano
   D. Kutofautisha uchumi na teknolojia
   E. Mwingiliano wa tamaduni tofauti tofauti

viii) Tamathali ya semi inayovifanya vitu visivyo na sifa ya ubinadamu vitende kama binadamu huitwa;
   A. Tashihisi
   B. Tashibiha
   C. Takriri
   D. Tasifida
   E. Taniaba

ix) Ni wahusika wapi katika tamthiliya ya Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe, Orodha na Kilio Chetu hawapaswi kuigwa na jamii zao kutokana na uovu wao?
   A. Padri James, Ngoswe na Anna
   B. Joti, Mary na Mama Mazoea
   C. Mitomingi, Anna na Mama Furaha
   D. Ngoswer, Joti na Padri James
   E. Anna, Mary na Mama Mazoea

x) Sherehe zifanywazo na jamii katika kipindi maalumu cha mwaka kwa lengo la kufundisha Maisha ya kundi fulani la wanajamii hujulikana kama;
   A. Kongozi
   B. Maghani
   C. Mivigha
   D. Matambiko
   E. Majigambo

2. Oanisha makossa ya kisarufi na kimantiki yaliyoko safu A kwa kuchagua herufi yenye aina ya kosa kutoka safu B, kisha andika herufi ya jibu sahihi uliyochagua katika kijitabu chako cha kujibia.

| SAFU 'A' | SAFU 'B' |
|---|---|
| i) Siku hizi Esther amenona sana --- | A. Kosa la kuongeza vitamkwa |
| ii) Mweusi paka panya amemkamata --- | B. Kosa la kuacha maneno |
| iii) Nikimariza kura nakwend kurara --- | C. Kosa la kimantiki |
| iv) Mimi silagi ugali --- | D. Kosa la kimatamshi |
| v) Baba ameondoka kazini --- | E. Kosa la kiuundo |
| vi) Nimefika nikamkuta hayupo --- | F. Kosa la kimsamiati |
| | G. Kosa la makabila |
| | H. Kosa la tafsiri sisi |

## SEHEMU B: (ALAMA 54)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

3. a) Eleza tofauti mbili (2) za kishazi huru na kishazi tegemezi.
   b) Tunga sentensi moja kwa kila muundo katika miundo ifuatayo;
   i) Kishazi huru kimoja
   ii) Kishazi huru kimoja na kishazi tegemezi kimoja
   iii) Vishazi tegemezi viwili
   iv) Kishazi tegemezi kimoja na vishazi huru viwili vilivyounganishwa na kiunganishi
   v) Vishazi tegemezi viwili na kishazi huru kimoja

4. a) Lahaja zina umuhimu mkubwa sana katika lugha. Eleza kwa ufupi dhima nne (4) za lahaja katika lugha ya Kiswahili.

   b) Usanifishaji wa lugha huwa na manufaa kwa lahaja pendekezwa wakati huo lahaja ghairi zikidhoofishwa. Kwa hoja tano (5) eleza ni kwa nini usanifishaji wa lahaja ya kiunguja ulisababisha lahaja nyingine kukosa mvuto.

5. a) Unaelewa nini kuhusu istilahi ya rejesta? Toa mifano miwili (2) kuthibitisha maelezo yako.
   b) Je, kuna umuhimu gani wa kuwa na rejesta? Eleza oja tano (5).

6. a) "Kuna wakati hutokea istilahi mbili kuwa na maana au majukumu ya namna moja". Thibitisha maelezo haya, kwa kutaja jina lingine pacha la kila neno katika maneno yafuatayo;
   i) Njeo
   ii) Shamirisho
   iii) Prediketa
   iv) Chagizo
   v) Kirai
   vi) Kikembe

   b) Maneno ya Kiswahili huwezakubadilika kuwa aina nyingine kulingana na matumiz au majukumu yake na mahali lilipo katika tungo. Tumia neno "<u>vizuri</u>" katika sentensi ili lifanye kazi kama;
   i) Kielezi – E
   ii) Kivumishi – V
   iii) Kiwakilishi – W

7. "Waandishi wengi wa kazi za kifasihi wamekuwa na misimamo thabiti ya kukaripia yale yaliyo kinyume na wao". Thibitisha kauli hii kupitia riwaya ya "Watoto wa Mama n'tilie," kwa hoja sita (6) tu.

8. a) Maneno ya Kiswahili hupatikana kwa njia mbalimbali. Dhihirisha njia zilizotumik kutokea kwa maneno yafuatayo;
   i) Kipimajoto
   ii) Masivina
   iii) Mwanamuziki
   iv) Malapa
   v) Mwanamuziki

   b) Maneno yafuatayo yametoholewa kutoka katika lugha mbalimbali za kigeni. Taja lugha lilipotokea neno na namna linavyoandikwa katika lugha yake ya asili.
   i) Elimu –
   ii) Shule –
   iii) duka
   iv) bahasha –

## SEHEMU C: (ALAMA 30)

Jibu maswali yote mawili (2) katika sehemu hii) swali la kumi (10) ni LAZIMA.

9. "Waandishi wa kazi za fasihi hutumia mitindo mbalimbali katika kazi zao". Dhihirisha maelezo hayo ukionesha jinsi waandishi wawili wa tamthiliya walivyofaulu katka kipengele cha mtindo kwa hoja tatu (3) kutoka kila tamthiliya.

10. "Wasanii wa ushairi huwa ni wazalendo na wanajamii halisi ambao hupenda kujadili uzalendo ulivyo muhimu katika uhai wa jamii zao". Thibitisha kauli haii kwa hoja tatu (3) kutoka kila tamthiliya.

11. "Waandishi wa kazi za kifasihi ni wakufunzi wazuri sana wa jamii zetu". Hakiki kauli hii kwa kutoa hoja tatu (3) kutoka katika riwaya kati ya mbili ulizosoma.

**ORODHA YA VITABU**

USHAIRI

- Wasakatonge - M. S. Khatibu (DUP)
- Malenga Wapya - TAKILUKI (DUP)
- Mashairi ya Chekacheka - T. A. Mvungi (EP & D LTD)

RIWAYA

- Takadini - Ben J. Hanson (MBS)
- Watoto wa Maman'tilie - E. Mbogo (HP)
- Joka la Mdimu -
- A. J. Safari (HP)

TAMTHILIYA

- Orodha - Steve Reynolds (M.A)
- Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe - E. Semzaba (ESC)
- Kilio Chetu - M. A. Foundation (TPH)